Makonnen, N., Tamba, H., Al Mahdi Abdulwahhab, M
Kimanzi, W., Good, E., & Oliver, E. (2026). #IJFAEAfric
Advancing Life-Saving First Aid Training Across Africa.
*International Journal of First Aid Education*, *9*(1), 1–7.
https://doi.org/10.25894/ijfae.3307

# #IJFAEAfrica: Kuendeleza Mafunzo ya Huduma ya Kwanza ya Kuokoa Maisha Barani Afrika

*Mwaliko kwa waelimishaji, wataalamu, na watafiti wa Afrika*

Nardos Makonnen, Hamza Tamba, Mai Hilal Al Mahdi Abdulwahhab, William Kimanzi, Esther Good, Emily Oliver

**MUHTASARI**

Jarida la Kimataifa la Elimu ya Huduma ya Kwanza (IJFAE) limeanzisha kampeni ya #IJFAEAfrica pamoja na mkusanyiko mpya wa machapisho ya Afrika ili kuinua elimu, utafiti, na vitendo vya huduma ya kwanza vinavyoongozwa na Waafrika. Katika jitihada za makusudi za kuendeleza elimu ya huduma ya kwanza kama nyenzo muhimu ya kuimarisha afya ya umma, hasa katika mazingira ya nchi zenye kipato cha chini na cha kati, kampeni yetu inalenga kukuza sauti za waandishi wa Afrika, kuongeza idadi ya machapisho, na kuiweka IJFAE kama jukwaa linaloaminika na linalofikika kwa urahisi kwa utafiti kuhusu elimu ya huduma ya kwanza, mafunzo ya jamii, na mwitikio wa mashuhuda wa matukio.

Ikiendeleza historia ya IJFAE ya kusaidia watafiti wanaochipukia kupitia warsha maalum za bure na ushauri elekezi, #IJFAEAfrica ni mwito mpya wa michango kutoka Afrika unaoonesha tathmini za programu, ubunifu wa mafunzo, miradi ya kijamii, na machapisho ya tafakari ya kitaalamu. Hili lichukulie kama jukwaa la pamoja ambapo taaluma inayoongozwa na Waafrika, vitendo vya kijamii, na utafiti wa kitaaluma vinakutana—na ambapo yeyote mwenye uzoefu, takwimu, au simulizi anaweza kupata msaada wa kuendeleza kazi yake hadi kuwa makala inayoweza kuchapishwa kwa msaada wa IJFAE.

Kuanzia mwaka 2026, #IJFAEAfrica itaongeza mchango kupitia msaada ulioboreshwa. Tutaunda mitandao ya mabalozi wa kikanda, kuanzisha ushirikiano na vyuo vikuu, kuandaa warsha za uandishi, na kupanua mwonekano wa kidijitali. Makala zitakazochapishwa kutoka Afrika au na waandishi wa Afrika zitachapishwa kikamilifu angalau katika lugha moja ya Kiafrika pamoja na Kiingereza.

Utafiti kutoka Afrika bado unawakilishwa kwa kiwango kidogo katika miongozo ya kimataifa. Huu ndio mchango wetu wa kukabiliana na hali hiyo. Tunakuhimiza kujiunga nasi kwa kutembelea mkusanyiko wa Afrika na ukurasa wetu wa uwasilishaji makala ili kusoma mwongozo kwa waandishi. Ikiwa una maswali au mawazo, unaweza kututumia barua pepe kupitia editor@firstaid-revolution.org.

**Submitted:** 24 February 2026 **Accepted:** 14 April 2026 **Published:** 12 May 2026

*International Journal of First Aid Education* is a peer-reviewed open access journal published by Aperio. © 2026 The Author(s). This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution 4.0 International License (CC BY 4.0), which enables reusers to distribute, remix, adapt, and build upon the material in any medium or format, so long as attribution is given to the creator.

OPEN ACCESS

Jarida la Kimataifa la Elimu ya Huduma ya Kwanza (IJFAE) ni jukwaa jumuishi na la upatikanaji huria (open-access) linalojitolea kuendeleza elimu ya huduma ya kwanza inayotegemea ushahidi duniani kote. Kama sehemu ya dhamira yetu ya kuleta usawa wa afya kimataifa na kuinua sauti ambazo mara nyingi hazisikiki, tunazindua kampeni ya #IJFAEAfrica ili kuangazia elimu ya huduma ya kwanza, utekelezaji, na tafiti zinazoongozwa na Waafrika.

Makala hii ya utangulizi inatambulisha #IJFAEAfrica pamoja na mkusanyiko wetu mpya wa Afrika (Africa Collection), na inawaalika waelimishaji, wataalamu wa vitendo, wanafunzi, na watafiti kote barani kushiriki kazi zao, hadithi zao, na ubunifu wao na dunia.

**Haja ya Kampeni**

Elimu ya huduma ya kwanza ni muhimu katika kujenga mfumo imara wa afya ya umma; huongeza maarifa na ujuzi wa vitendo, hata kwa watu wasiokuwa na mafunzo rasmi ya kitabibu (Ygiyeva et al., 2024). Hata hivyo, licha ya umuhimu wake mkubwa—hasa katika mazingira ya nchi zenye kipato cha chini na cha kati—tafiti kuhusu elimu ya huduma ya kwanza kutoka nchi za Afrika bado hazijawakilishwa vya kutosha. IJFAE ilianzishwa kama jukwaa jumuishi na la upatikanaji huria kwa ajili ya kuendeleza elimu ya huduma ya kwanza inayotegemea ushahidi duniani kote, lakini kwa sasa kuna mapungufu kadhaa ya uonekana na ushiriki yanayopunguza upeo na athari zake barani Afrika.

Mapungufu haya yanajumuisha uelewa mdogo kuhusu jarida hili miongoni mwa waelimishaji wa huduma ya kwanza, mashirika yasiyo ya kiserikali, na taasisi za mafunzo; idadi ndogo ya machapisho ya tafiti zinazoongozwa na Waafrika; pamoja na kukosekana kwa mitandao ya mabalozi wa ndani na ushirikiano rasmi na vyuo vikuu.

Matokeo yake, maarifa muhimu ya ndani, ubunifu, na mbinu zinazozingatia muktadha wa eneo husika hubaki bila kushirikishwa ipasavyo, hali inayoongeza pengo la usawa kuhusu ni ushahidi upi unaotumika kuunda viwango vya kimataifa vya huduma ya kwanza. Kampeni zilizoratibiwa kwa umakini na kimkakati zimeonyesha mafanikio katika kukabiliana na changamoto kama hizi katika nyanja za afya ya umma, elimu, na usalama wa jamii (AlSabah et al., 2018). Zinapobuniwa kwa uangalifu, kampeni zinaweza kuongeza uelewa, kuimarisha mifumo, na kuhamasisha rasilimali.

Kutokana na hitaji la haraka la kuinua sauti za Waafrika katika tafiti za elimu ya huduma ya kwanza—pamoja na msisitizo unaoongezeka duniani kuhusu uingiliaji wa watu wa kawaida (bystander intervention) na mwitikio wa dharura unaotegemea jamii—huu ni wakati muhimu wa kuzindua kampeni maalum ya kuongeza uonekana, umuhimu, na athari za IJFAE barani Afrika.

Ndiyo maana tumezindua #IJFAEAfrica, pamoja na *The Africa Collection*, ambayo inajumuisha makala zilizotafsiriwa kikamilifu katika angalau lugha moja ya Kiafrika mbali na Kiingereza. Michango ya awali inajumuisha makala kuhusu mada mbalimbali, kama vile juhudi za *kuzuia damu* nchini Kenya, pamoja na tafiti zinazochunguza maarifa, mitazamo, na vitendo vya wazazi kuhusiana na uhifadhi salama na utupaji wa dawa nchini Libya.

**Kufafanua Madhumuni ya Kampeni**

Lengo kuu la kampeni ya #IJFAEAfrica ni kukuza na kuonekana kwa waandishi na tafiti kutoka Afrika kwa kuiweka IJFAE kama jukwaa linaloaminika, linalopatikana kwa urahisi, na lenye umuhimu kwa utafiti na ubunifu wa elimu ya huduma ya kwanza katika muktadha wa Afrika. Kuongeza uelewa kwamba IJFAE ni bure kusoma na bure kuchapisha kunaweza kupunguza vikwazo vya kimuundo, hasa katika maeneo ambapo upatikanaji wa ufadhili wa tafiti ni changamoto.

IJFAE ina historia ya kusaidia waandishi wanaochipukia, wakiwemo watafiti wa ngazi za awali, kupitia warsha za mtandaoni zisizolipiwa, kozi fupi, na programu za uongozi (mentorship) katika mbinu za utafiti,

uandishi wa kisayansi, na elimu ya huduma ya kwanza. Mipango hii imeundwa ili kuimarisha uwezo na kujiamini kwa waandishi, na tunakusudia kuendeleza jitihada hizi kadri mtandao wetu wa mabalozi wa kujitolea unavyoendelea kukua.

Lengo muhimu la kampeni ni kuongeza idadi ya machapisho kutoka kwa waandishi wa Afrika, hasa yale yanayolenga elimu ya huduma ya kwanza, mifumo ya mafunzo, mwitikio wa watu wa kawaida (bystander response), na afua za ngazi ya jamii zinazozingatia hali halisi za maeneo husika. Tunakaribisha kwa upekee miswada kama tathmini za programu, ubunifu katika mafunzo, miradi ya kijamii, tafiti za utekelezaji (implementation case studies), miradi inayoongozwa na wanafunzi, pamoja na maandiko ya tafakari ya kitaaluma yanayobadilisha uzoefu wa ndani kuwa maarifa ya pamoja.

Kampeni hii pia inatoa fursa ya kuiweka elimu ya huduma ya kwanza kama nguzo muhimu ya afya ya umma: kuongeza uelewa, mafunzo, na ushiriki vina uhusiano wa karibu na vinaweza kuleta mabadiliko ya tabia endapo vitaongozwa na mbinu za huduma ya kwanza zinazotegemea ushahidi pamoja na tafsiri ya tafiti katika ufundishaji na mafunzo. Kwa njia hii, hatua zote za (*Mlolongo wa Tabia za Kuokoa Maisha)* zinaweza kutekelezwa kwa ufanisi.

Kwa kiwango kipana zaidi, kampeni hii inalenga kuathiri mifumo na sera kwa kuonyesha athari ya kuokoa maisha ya uingiliaji wa watu wa kawaida (bystander intervention) pamoja na umuhimu wa elimu bora ya huduma ya kwanza katika kuimarisha njia za huduma za dharura. Kwa kuinua ushahidi unaotokana na mazingira ya Afrika, kampeni inaweza kusaidia utetezi wa ongezeko la uwekezaji katika mafunzo, elimu ya jamii, na uimarishaji wa uwezo wa taasisi.

Walengwa wetu ni pamoja na:

- Wataalamu wa masuala ya kitaaluma na watendaji ambao wanaweza kuwa waandishi, wakaguzi (reviewers), na washirika wa utafiti
- Vyuo vikuu na taasisi za mafunzo
- Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na taasisi za kitaaluma zinazohusika na huduma ya kwanza na huduma za dharura
- Watunga sera na viongozi wa mifumo ya afya

Ikiwa unaendesha programu ya mafunzo ya eneo husika, unaratibu wahudumu wa afya ya jamii, au unafundisha huduma ya kwanza kwa wanafunzi, tayari una uzoefu, data, na hadithi ambazo zinaweza kugeuzwa kuwa makala ya kitaaluma yenye uwezo wa kuchapishwa kwa msaada wetu.

**Mafunzo kutoka kwa Kampeni Zingine Zilizofanikiwa**

Kampeni nyingi za afya ya umma duniani—kama zile zinazolenga kinga ya magonjwa ya kuambukiza, kuongeza upokeaji wa chanjo, na usambazaji wa miongozo ya kitaalamu—zinatoa mafunzo muhimu kwa juhudi hii. Zinadhihirisha jinsi uratibu wa ujumbe, ushirikishwaji wa jamii, na (tafsiri za ushahidi) vinavyoweza kuleta athari endelevu (Ekezie et al., 2024). Tafiti zinazochunguza mikakati ya mawasiliano ya chanjo na michakato ya uundaji wa miongozo zinaonyesha umuhimu wa kuziba mapengo ya ushahidi kupitia mbinu jumuishi zinazozingatia muktadha wa jamii husika. Katika mifano mingine, elimu ya CPR kwa wingi imeonyesha mafanikio kupitia kanuni ya “cascade model”, ambapo (wakufunzi wakuu) hufundisha wakufunzi wengine, nao baadaye hufundisha (waokoaji wa kawaida) (Strömsöe et al., 2010). Mbinu hizi zinaonyesha kuwa athari kubwa hupatikana pale ambapo maarifa hayabaki katika ngazi ya kitaalamu pekee, bali husambazwa kwa njia ya kimfumo hadi ngazi ya jamii.

Mifano hii inaonyesha nguvu ya (ufikiaji wa kimakusudi), (kujenga uwezo), na (upatikanaji wa majukwaa) katika kubadilisha ni nani anazalisha na kunufaika na maarifa. Pia inaonesha kwamba kampeni zinazoweka sauti za wenyeji katikati na kukuza

ushirikiano, badala ya kutegemea usambazaji wa taarifa wa upande mmoja, zina uwezekano mkubwa zaidi wa kuleta athari endelevu. Kwa #IJFAEAfrica, hili linamaanisha kuipa kipaumbele lugha za Kiafrika, (mabalozi wa ndani), na mada zinazoongozwa na jamii, pamoja na kubuni kwa makusudi shughuli zinazowawezesha waelimishaji na watendaji kuathiri si tu majibu ya utafiti, bali pia maswali yanayoulizwa na aina ya ushahidi unaoshirikishwa.

Kote barani Afrika, ujuzi wa huduma ya kwanza unaookoa maisha unafundishwa kwa watu wa kawaida katika vituo vya mafunzo vya ndani na wataalamu wa maeneo husika. Kupitia #IJFAEAfrica, kazi kama hii inaweza kuandikwa, mbinu bora kushirikishwa, na mbinu mpya kujaribiwa na kuboreshwa kote Afrika na hata nje ya bara.

**#IJFAEAfrica ni nini?**

Dira yetu ni rahisi: kuifanya IJFAE kuwa rasilimali kuu ya kitaaluma na ya vitendo kwa utafiti na ubunifu wa elimu ya huduma ya kwanza barani Afrika. Hadithi ya kampeni hii inasisitiza IJFAE kama jukwaa linalothamini usomi unaoongozwa na Waafrika, linalosaidia waandishi chipukizi, na linalounganisha taaluma, utekelezaji wa vitendo, na uhamasishaji wa jamii. Ujumbe mkuu unalenga kuimarisha uonekano, uaminifu, na ushirikiano ndani ya sekta za afya, elimu, na huduma za dharura. Badala ya kuiweka jarida kama mamlaka ya nje, kampeni inaielekeza IJFAE kama nafasi ya pamoja ya kujifunza, kubuni, na kuleta athari halisi.

#IJFAEAfrica itazinduliwa mwaka 2026, ikiwa na mkazo katika mafunzo ya huduma ya kwanza, (huduma za kabla ya hospitali), na utafiti unaohusu huduma za dharura za kitabibu.

**Shughuli na vipaumbele vya awali**

Ili kutimiza maono haya, #IJFAEAfrica itazingatia vipaumbele vifuatavyo:

- Kuanzisha mitandao ya mabalozi wa kikanda ili kuiunganisha IJFAE na waelimishaji wa ndani, taasisi, na jamii
- Kujenga ushirikiano na vyuo vikuu na taasisi za mafunzo ili kuingiza utafiti wa elimu ya huduma ya kwanza na maudhui ya IJFAE katika ufundishaji na tathmini
- Kuandaa warsha za uandishi na mitandao ya mtandaoni (webinars) zilizoandaliwa mahsusi kwa waandishi wapya na wanaochipukia, ikiwemo wale ambao hawajawahi kuchapisha kabla
- Kutumia mitandao ya kijamii na mitandao ya kitaaluma kuongeza uonekano wa kidijitali, kukuza maudhui ya lugha za Kiafrika, na kushiriki hadithi za mafanikio
- Kukuza ushirikiano wa taaluma mbalimbali na sekta tofauti unaounganisha waelimishaji wa huduma ya kwanza na afya ya umma, huduma za dharura, na watunga sera

**Vipaumbele vya mwaka wa kwanza**

Katika mwaka wa kwanza wa kampeni, shughuli muhimu zitajumuisha:

- Kuandaa warsha za uandishi za mtandaoni zilizoelekezwa kwa makundi maalum
- Kuajiri mabalozi kutoka angalau nchi 5 za Afrika
- Kuangazia angalau makala 3 zinazoongozwa na Waafrika ndani ya *Mkusanyiko wa Afrika*
- Kushirikiana na angalau vyuo vikuu 2 kuingiza maudhui ya IJFAE katika mitaala yao

Ushirikiano wa jamii na washirika wa kitaaluma utakuwa muhimu kuhakikisha umuhimu na uendelevu wa kampeni. Tutafuatilia idadi na aina ya ushirikiano, kuchunguza kama ushirikiano na vyuo vikuu unaongeza fursa za mafunzo ya utafiti na ushiriki wa wanafunzi katika elimu ya huduma ya kwanza, pamoja na kufuatilia ujumuishaji wa maudhui ya IJFAE katika programu za kitaaluma. Kupima mafanikio ya kazi hii kwa muda kutasaidia kuelekeza

juhudi kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa zaidi na kujifunza kadri tunavyoendelea.

Pia tunapanga kushirikisha taarifa za mara kwa mara kuhusu maendeleo ya kampeni kupitia tovuti ya IJFAE, mitandao ya kijamii, na makala zijazo za uhariri, ili wachangiaji waweze kuona jinsi mchango wao unavyochangia harakati pana zaidi.

## Mawasiliano na Usambazaji

Utekelezaji wenye mafanikio utahitaji mkakati wa mawasiliano ulio wazi unaotumia washirika wa taasisi, vyama vya kitaaluma, mitandao ya vyuo vikuu, na majukwaa ya kidijitali. Juhudi za usambazaji zitatumia njia zote za kitaaluma (kama makala za jarida, mawasilisho kwenye mikutano ya kisayansi, na ushirikiano wa taasisi) pamoja na njia zisizo rasmi (kama mitandao ya kijamii, mitandao ya jamii, na makundi ya wataalamu wa vitendo). Kutafsiri ujumbe muhimu katika lugha zinazotumika zaidi barani Afrika na kuubinafsisha kulingana na hadhira tofauti kutakuwa kiini cha mkakati huu.

Kupitia juhudi za ushirikiano zilizopangwa vizuri, kampeni hii inaweza kuongeza ushiriki, kuimarisha ushahidi, na kuboresha elimu ya huduma ya kwanza pamoja na matokeo yake barani Afrika. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba waelimishaji wa huduma ya kwanza, wahudumu wa afya wa jamii, wanafunzi, na wataalamu wa huduma za dharura kote barani Afrika wanaiona IJFAE kama nyumbani kwa mawazo yao, ubunifu wao, na utafiti wao.

## Jinsi Unavyoweza Kushiriki katika #IJFAEAfrica

Timu ya Uhariri ya IJFAE inayojitolea kwa hiari inawaalika wasomaji wake kuunga mkono kampeni ya #IJFAEAfrica. Iwe wewe ni mtafiti mwenye uzoefu, mkufunzi wa jamii, mwanafunzi, au mtaalamu wa vitendo, kuna nafasi yako katika harakati hizi.

## Njia za kushiriki

Kuna njia mbalimbali za kushiriki, zikiwemo:

**Kushiriki kazi yako:** Tuma miswada inayoelezea programu zako, tathmini, ubunifu katika mafunzo, au mafunzo uliyojifunza kutoka kwenye utekelezaji wa vitendo.

**Kujifunza na kujenga ujuzi:** Jiunge na warsha zetu za mtandaoni na fursa za ushauri (mentorship) ili kukuza ujuzi katika usanifu wa utafiti, uchambuzi wa data, na uandishi wa kisayansi.

**Kuwasiliana na kushirikiana:** Shirikiana nasi kama chuo kikuu, taasisi ya mafunzo, NGO, au chombo cha kitaaluma, au jitolee kama mkaguzi wa makala (reviewer) au balozi wa kampeni.

## Hatua za kuanza

Unaweza kuanza kwa kuchunguza *Mkusanyiko wa Afrika* na (kutembelea ukurasa wa mawasilisho) ili kusoma miongozo ya waandishi. Ikiwa una maswali au mawazo, unaweza kutuma barua pepe kwa: **editor@firstaid-revolution.org**

Hata kama hujawahi kuchapisha kabla, au Kiingereza si lugha yako ya kwanza, tunakuhimiza kuwasiliana nasi. Rasimu zisizo kamili na mawazo ya awali yanakaribishwa; dhamira yetu ya usawa inajumuisha kuwasaidia waandishi kuunda na kuimarisha kazi zao, si tu kuzitathmini kama maandiko yaliyokamilika.

## Jiunge na harakati

Tunakualika kuunga mkono #IJFAEAfrica kwa kushiriki makala hii na wenzako, wanafunzi, na marafiki; kutufuata kwenye LinkedIn, Instagram, YouTube, TikTok @ijfae, na Facebook; pamoja na kutuunganisha na taasisi au mitandao inayoweza kutaka kushirikiana.

Pamoja, tunaweza kujenga msingi imara wa ushahidi unaoongozwa na Afrika katika elimu ya huduma ya kwanza na kuchangia kuokoa maisha kote barani.

Hamza Tamba, William Kimanzi na Mai Hilal Al Mahdi Abdulwahhab wanatoa elimu ya huduma ya kwanza barani Afrika. Nardos Makonnen na Esther Good wanafanya kazi na watoa huduma za afya barani Afrika.

# Marejeleo

AlSabah, S., Al Haddad, E., & AlSaleh, F. (2018). Stop the bleed campaign: A qualitative study from our experience from the middle east. *Annals of medicine and surgery (2012)*, *36*, 67–70. https://doi.org/10.1016/j.amsu.2018.10.013

Ekezie, W., Igein, B., Varughese, J., Butt, A., Ukoha-Kalu, B. O., Ikhile, I., & Bosah, G. (2024). Vaccination Communication Strategies and Uptake in Africa: A Systematic Review. *Vaccines*, *12*(12), 1333. https://doi.org/10.3390/vaccines12121333

Strömsöe, A., Andersson, B., Ekström, L., Herlitz, J., Axelsson, A., Göransson, K. E., Svensson, L., & Holmberg, S. (2010). Education in cardiopulmonary resuscitation in Sweden and its clinical consequences. *Resuscitation*, *81*(2), 211–216. https://doi.org/10.1016/j.resuscitation.2009.10.014

Ygiyeva, D., Pivina, L., Messova, A., Omarov, N., Batenova, G., Jamedinova, U., & Dyussupov, A. (2024). Evaluating the Effectiveness of a First Aid Training Programme for Individuals Without a Background in Medical Education. *Advances in medical education and practice*, *15*, 773–782. https://pmc.ncbi.nlm.nih.gov/articles/PMC11345019/pdf/amep-15-773.pdf